JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

ISO 9001:2015 CERTIFIED

# TAARIFA KWA UMMA

## WITO WA KUTOA MAONI KWENYE RASIMU YA WARAKA WA UGAWAJI WA MASAFA YA MAWASILIANO YA SIMU NA INTANETI KATIKA BENDI 3600-3800 MHz

Kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Sura ya 172 na Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta, Sura ya 306 ya Sheria za Tanzania, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ina jukumu la kupanga, kuidhinisha, kugawa, kutoa, kuchukua, kusimamisha matumizi, kufuta au kwa namna yoyote ile kurekebisha mgawo wa masafa miongoni mwa watumiaji au wenye leseni za masafa ya mawasiliano.

Katika kutekeleza majukumu hayo, mnamo tarehe 18 Disemba 2024 TCRA ilitoa taarifa kwa umma na wadau kuwa imepanga kugawa masafa ya bendi 3600-3800 MHz katika vitalu vinne (4) vya 1x50 MHz vilivyotengwa kwa ajili ya huduma za mawasiliano ya simu na intaneti kwa njia ya ushindani.

Kuelekea ugawaji wa masafa husika, TCRA inawaalika wadau wa sekta ya mawasiliano ya simu na umma kwa ujumla kutoa maoni, maswali na ushauri kwa njia ya maandishi kwenye Rasimu ya Waraka wa Ugawaji wa Masafa ya Mawasiliano ya Simu na Intaneti katika bendi 3600-3800 MHz. Waraka huo umeainisha taratibu mbalimbali ikiwemo vigezo vya ushiriki, sifa za waombaji, kiwango cha juu cha masafa kinachoweza kugawiwa (Spectrum Cap) na bei ya kuanzia ya ugawaji wa masafa (Reserve Price).

Rasimu ya Waraka inapatikana katika tovuti ya TCRA kupitia www.tcra.go.tz.

Ushauri, maoni na maswali yawasilishwe kwa njia ya maandishi kabla ya **saa kumi kamili alasiri, Jumatano tarehe 23 Aprili 2025,** kupitia barua pepe **spectrum.auction@tcra.go.tz** au kwa njia ya posta kwenda kwa Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Ghorofa ya Nane Jengo la Mawasiliano, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma, S.L.P 474, 14414 Dar es Salaam.

Imetolewa tarehe **03 Februari, 2025.**

Dkt. Jabiri K. Bakari

**MKURUGENZI MKUU**

Jengo la Mawasiliano, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma, S. L. P 474, 14414 DAR ES SALAAM, TANZANIA.
**Simu:** +255 22 2199760-9 / +255 22 2412011-2 / +255 784558270-1 **Nukushi:** +255 22 2412009-10
**Barua pepe:** barua@tcra.go.tz, dg@tcra.go.tz, **Tovuti:** www.tcra.go.tz